

**TANGAZO LA ZABUNI YA UGAVI WA MAGUNIA YA KAHAWA SAFI (JUTE BAGS) MSIMU 2026/2027**

Zabuni na: KCU/G/2026/2027/03

1. KCU (1990) Ltd imetenga fedha kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kimkataba na mtoa huduma ya ugavi wa magunia ya kahawa safi (Jute bags) kwa msimu 2026/2027. Kampuni/Shirika/Mtu binafsi anayotambulika anakaribishwa kuleta maombi ya zabuni hii ili kutoa huduma ya ugavi wa magunia ya kahawa safi (Jute bags)
2. Magunia ya kahawa Safi (Clean Coffee) yawe na sifa kama ifuatavyo:-
  - Aina - Jute bags
  - Kipimo - Inchi 44 kwa inchi 26.5
  - Uzito - Gram 848
  - Ujazo - kilo 60 za kahawa safi
  - Idadi - 42000
3. Mwombaji anaweza kufika katika ofisi ya manunuzi KCU ili kuona sampuli ya gunia linalohitajika.
4. Mwombaji aeleze ni ndani ya muda gani anao uwezo wa kuwasilisha vifungashio hivyo kuanzia siku ya kupewa agizo (order).
5. Mwombaji ataje bei ya kila gunia kwa kufikisha kwenye ghala la KCU (1990) Bukoba. **(Eleza kama bei ni pamoja na VAT au bila VAT)**
6. Mwombaji aambatishe nakala ya wasifu wa kampuni/shirika
7. Mwombaji aambatishe nakala ya usajili wa kampuni.
8. Kampuni/Shirika/Mtu ni lazima aambatishe nakala ya leseni ya biashara, TIN na VRN.
9. Mwombaji aambatishe nakala zinaonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya.
10. Ombi la zabuni liwe na jina, anwani halisi ya mwombaji na mahali Ofisi ilipo (Physical address)
11. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**
12. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 4-11 vilivyo tajwa hapo juu.
13. Bahasha ya maombi ifungwe vizuri kwa Lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI YA ZABUNI YA UGAVI WA MAGUNIA YA KAHAWA SAFI (EXPORT JUTE BAGS)" MSIMU 2026/2027** kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,  
KCU (1990) LTD,  
P.O BOX 5,  
BUKOBA.
14. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni
15. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.

